

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ مَأْمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لِيَسْتَعْلَمُنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَسْتَخَلَفَ
الَّذِينَ مِنْ قَلْبِهِمْ وَيَمْكُنُ لَهُمْ دِينُهُمُ الَّذِي أَرَضَى لَهُمْ وَلَيَسْتَدِيلُهُمْ مِنْ بَعْدِ حَرْقَفِهِمْ أَمَّا
يَعْبُدُونَ فَلَا يُشَرِّكُونَ فِي شَيْءٍ وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الْقَسِيقُونَ



Jumatatu, 17 Muhamarram 1444 H

15/08/2022 M

Na: H.T.L 1444 / 01

Tanzia ya Mbebaji Ulinganizi

(مِنَ الْمُؤْمِنِينَ رَجُلٌ صَدَقَوْ مَا عَاهَدُوا اللَّهُ عَلَيْهِ فَنِئُهُمْ مِنْ قَضَى نَجْهَةٍ
وَمِنْهُمْ مَنْ يَتَنَظَّرُ وَمَا يَنْهَا تَبَدِيلًا)

“Miiongoni mwa Waumini wapo watu walio timiza waliyo ahidiana na Mwenyezi Mungu. Baadhi
yao wamekwisha kufa, na baadhi wanangojea, wala hawakubadilisha (ahadi) hata kidogo.” [Al-
Ahzab: 23]
(Imetafsiriwa)

Hizb ut Tahrir katika Wilayah ya Lebanon inamuomboleza kaka mbeba dawah, Jamal Suleiman Abu Khaled, aliyeferiki alfajiri ya leo, Jumatatu, 17 Muhamarram 1444 H, sawia na 15/08/2022, akiwa na umri wa miaka 59.

Abu Khaled Suleiman, mmoja wa watu wa mwanzo wa ulinganizi huu katika miji ya Sidon na Tiro na viunga vyake, aliibeba dawah kwa uaminifu na ikhlasi. Sisi tunamchukulia vivyo hivyo, na Mwenyezi Mungu ndiye mwenye hesabu yake, na hatumsifu yeyote mbele ya Mwenyezi Mungu, katika siku zake ngumu na dhurufu zenyek kiza kikubwa, na dawah ilimjua tu kama mtu mwenye tabia njema, mshikamano mwema, makini na mvumilivu ndani yake, akiipenda dawah na kizazi chake kichanga.

Abu Khaled alikuwa mwenye utambuzi wa kifikra, mwenye maoni yaliyo wazi, sahihi, na ufahamu sawasawa. Kijana mmoja alimuuliza siku moja: Ulinganizi huu tutaubeba kwa muda gani? Akajibu: “Mpaka kufa, na akasoma maneno ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

(وَاعْبُدْ رَبَّكَ حَتَّىٰ يَأْتِيكَ الْيَقِинُ) “Na muabudu Mola wako Mlezi mpaka ikufikie Yakini.” [Al-Hijr:99]” na ndivyo alivyokuwa. Hakubweteka katika wajibu au kazi yoyote, hata iwe nyingi kiasi gani, hadi siku za mwisho za uhai wake, Mwenyezi Mungu (swt) amrehemu.

Abu Khaled alifanya kazi ya kusimamisha Khilafah, na aliiiona imesimama mbele yake, akiwa na yakini na ahadi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na bishara njema ya Mtume Wake, rehema na amani zimshukie yeye na jamaa zake.

Jicho linatokwa na machozi, moyo unahuzunika, na sisi tumehuzunishwa na kutengana nawe, na hatusemi ila tu yanayompendeza Mola wetu. (إِنَّ اللَّهَ وَإِنَّ إِلَيْهِ رَاجُونَ) “Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake Yeye hakika tutarejea.” [Al-Baqara:156].

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir
katika Wilayah Lebanon**